JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

UHURU NA UMOJA

# TAARIFA YA MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI MKOA WA KATAVI TOKA MWAKA 2021 HADI MWEZI FEBRUARI, 2026.









IMEANDALIWA NA:
OFISI YA MKUU WA MKOA,
S.L.P 235,
MPANDA - KATAVI.
SIMU NA: +255 25 2957108
FAX NA: +255 25 2957108
Barua pepe: ras.katavi@tamisemi.go.tz

FEBRUARI,2026

# YALIYOMO


1.0 Utangulizi........................................................1

1.1 Eneo la Mkoa................................................1

1.1.2 Maeneo ya Kiutawala................................1

1.1.3. Idadi ya Watu..........................................1

1.1.4.Majukumu ya Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji........................................1

2.0 Sekta ya Uwekezaji .......................................2

2.1. Wilaya ya Tanganyika.................................2

2.2. Wilaya ya Mlele.........................................3

2.3. Eneo la Uwekezaji SIDO..............................5

3.0. SEKTA YA VIWANDA.....................................5

4.0. SEKTA YA BIASHARA.....................................11

5.0 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA..................19

6.0 Wakala wa Vipimo (WMA...........................20

7.0 SEKTA YA BANDARI .......................................22

8.0 SEKTA YA USAFIRI WA ANGA..............................24

9.0 SEKTA YA MADINI...........................................25

10. SHIRIKA LA VIWANGO (TBS)..............................27

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Eneo la Mkoa

Mkoa wa Katavi ulianzishwa rasmi tarehe 01 Machi, 2012 kupitia **Tangazo la Serikali Na. 72.** Mkoa una ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 47,527 ambapo eneo la nchi kavu ni kilomita za mraba 45,843 na eneo la maji ni kilomita za mraba 1,684. Katika eneo la nchi kavu eneo lifaalo kwa Kilimo ni Hekta 932,136 na eneo la misitu ni Hekta 3,142,232.

### 1.2 Maeneo ya Kiutawala

Mkoa una jumla ya Wilaya tatu (3) ambazo ni Wilaya ya Mpanda, Mlele na Tanganyika. Halmashauri zipo tano (5) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe. Tarafa zipo 10, Kata 51, Vijiji 130, Mitaa 43 na Vitongoji 681.

### 1.3 Idadi ya Watu

Kwa mwaka 2026 Mkoa wa Katavi unakisiwa kuwa na jumla ya watu 1,292,992 ikiwa wanaume ni 642,691 na wanawake ni 650,301. Hivyo ikadariwa wakazi 140,034 wameongezeka baada ya sensa ya mwaka 2022 ambapo matokeo ya sensa yanaonyesha Mkoa wa Katavi unajumla ya watu 1,152,958.

### 1.4 Majukumu Makuu ya Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

Majukumu makuu ya Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni pamoja na kusimamia, kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kukuza na kuendeleza maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji ndani ya Mkoa.

## 2.0. SEKTA YA UWEKEZAJI

Mkoa wa Katavi umebarikiwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji, baadhi ya fursa hizi ni uwepo wa ardhi yenye rutuba kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji, uwepo wa madini ya aina mbalimbali, uwepo wa vivutio vingi vya utalii hasa kutokana na uwepo wa hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Pia fursa ya uwepo wa ziwa Tanganyika kwa ajili ya uwekezaji kwenye uvuvi na vyombo vya usafiri, fursa ya uwepo wa bandari ya Karema ambayo ni ya kisasa, fursa za uanzishaji wa viwanda mbalimbali kama vile viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo, viwanda vya mabati, vinywaji, sementi nk. Ili kuhamasisha na kuvutia wawekezaji, Mkoa wa Katavi umetenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uwekezaji kama ifuatavyo;

### 2.1. Wilaya ya Tanganyika

i. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imetenga ekari 115,000 katika eneo la Luhafwe kwa ajili ya uwekezaji kwenye kilimo na viwanda. Ekari zilizopata wawekezaji ni 56,479, ambapo jumla ya wawekezaji 26 wapo katika hatua mbalimbali za kuanza uwekezaji. Baadhi ya wawekezaji wakubwa waliomilikishwa ardhi na wapo katika hatua za awali za uwekezaji ni SEEDLAND, MERU AGRO TOUR CONSULTANT LTD, ASA na na NATIONAL LAND COMPANY LTD. Aidha, jumla ya ekari 58,521 zimetengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama makazi na hifadhi ya misitu.

ii. Halmashauri imetenga eneo la ekari 206 katika maeneo ya Kabungu, Mpanda ndogo, Karema, Ifukutwa na Itetemya ambazo zitatumika katika uwekezaji wa viwanda.

iii. Pia zipo ekari 3,160 za watu binafsi ambazo mwekezaji anaweza kuingia kwenye makubalia no na wenye maeneo hayo.

Mchanganuo wa ardhi kwa ajili matumizi ya uwekezaji na matumizi mengine umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

| **Ekari zilizotengwa** | **Umiliki wa eneo** | | Ekari zilizopata wawekezaji | Ekari zilizotengwa kwa matumizi mengine | Ekari ambazo hazijapata wawekezaji | Idadi ya wawekezaji waliofanya uwekezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Watu Binafsi | | | | |
| 115,000 | 115,000 | 3,160 | 56,479 | 58,521 | 3,160 watu binafsi | 27 |

***Chanzo:*** *Taarifa kutoka Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri 2025/2026.*

Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ambazo zipo katika Wilaya ya Mlele zimetenga maeneo ya uwekezaji kama ifuatavyo;

- Ekari 22 zimetengwa eneo la Inyonga Halmashauri ya Mlele kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda.
- Ekari 120.72 zimetengwa eneo la Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo.
- Ekari 51.25 zimetengwa eneo la Kitupa - Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali katika sekta ya biashara.
- Ekari 26.37 zimetengwa eneo la Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali katika sekta za Elimu na Afya.

Mchanganuo wa ardhi kwa ajili matumizi ya uwekezaji na matumizi mengine umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

| **Ekari zilizotengwa** | **Umiliki wa eneo** | | Ekari zilizopata wawekezaji | Ekari zilizotengwa kwa matumizi mengine | Ekari ambazo hazijapata wawekezaji | Idadi ya wawekezaji waliofanya uwekezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Watu Binafsi | | | | |
| 115,000 | 115,000 | 3,160 | 56,479 | 58,521 | 3,160 watu binafsi | 27 |

***Chanzo:*** *Taarifa kutoka Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri 2025/2026.*

## 2.2. Wilaya ya Mlele

Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ambazo zipo katika Wilaya ya Mlele zimetenga maeneo ya uwekezaji kama ifuatavyo;

- Ekari 22 zimetengwa eneo la Inyonga Halmashauri ya Mlele kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda.
- Ekari 120.72 zimetengwa eneo la Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo.
- Ekari 51.25 zimetengwa eneo la Kitupa - Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali katika sekta ya biashara.
- Ekari 26.37 zimetengwa eneo la Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali katika sekta za Elimu na Afya.

Mchanganuo wa ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

| **Ekari zilizotengwa** | **Umiliki wa eneo** | | Ekari zilizopata wawekezaji | Ekari ambazo hazijapata wawekezaji | Idadi ya wawekezaji waliofanya uwekezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Watu Binafsi | | | |
| 220.34 | 110.43 | 110 | 110 | 90 .43 | 103 |

***Chanzo:*** Taarifa kutoka Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri 2025/2026.

## 2.3. Eneo la Uwekezaji SIDO

SIDO Mkoa wa Katavi imetenga eneo la ekari 21 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vya aina mbalimbali. Pia SIDO inamajengo yanayokodishwa kwa ajili ya viwanda vidogo na chumba cha baridi (coldroom) kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa. Wawekezaji wanakaribishwa kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kuwekeza kwenye eneo na majengo ya SIDO.

## 3.0. SEKTA YA VIWANDA

Idadi ya viwanda katika Mkoa wa Katavi imeongezeka kutoka 873 mwaka 2021 hadi 1,934 mwezi Februari, 2026. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni 7, viwanda vya kati ni 25, viwanda vidogo ni 555, na viwanda vidogo sana ni 1,337, jumla ya watu walioajiriwa katika viwanda hivyo ni 6,378.

Mchanganuo wa viwanda kwa kila Halmashauri umeoneshwa katika jedwali lifuatavyo;

| **Halmashauri** | **Kundi la Kiwanda** | **Idadi ya Wafanya kazi** | **Mtaji Uliowekezwa katikaMitambo (TSH** | **Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa** | **Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda** |
|---|---|---|---|---|---|
| **NSIMBO DC** | Kiwanda Kidogo Sana (Micro Enterprise) | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 228 | 460 |
| | Kiwanda Kidogo (Small Enterprise) | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 126 | 248 |
| | Kiwanda cha Kati (Medium Enterprise) | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 4 | 39 |
| | Kiwanda Kikubwa (LargeEnterprise) | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 2 | 235 |
| **Jumla** | | | | **360** | **982** |

| Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanya kazi | Mtaji Uliowekezwa katikaMitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| **MPANDA MC** | Kiwanda Kidogo Sana (Micro Enterprise) | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 470 | 1,802 |
| | Kiwanda Kidogo (Small Enterprise) | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 67 | 511 |
| | Kiwanda cha Kati (Medium Enterprise) | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 7 | 41 |
| | Kiwanda Kikubwa (Large Enterprise) | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 2 | 86 |
| **Jumla** | | | | **546** | **2,440** |

| Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanya kazi | Mtaji Uliowekezwa katikaMitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| **TANGA NYIKA DC** | Kiwanda Kidogo Sana (Micro Enterprise) | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 311 | 705 |
| | Kiwanda Kidogo (Small Enterprise) | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 281 | 552 |
| | Kiwanda cha Kati (Medium Enterprise) | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 3 | 82 |
| | Kiwanda Kikubwa (Large Enterprise) | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 1 | 59 |
| **Jumla** | | | | **616** | **1,398** |

| Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanya kazi | Mtaji Uliowekezwa katikaMitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| **MLELE DC** | Kiwanda Kidogo Sana (Micro Enterprise) | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 152 | 382 |
| | Kiwanda Kidogo (Small Enterprise) | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 34 | 244 |
| | Kiwanda cha Kati (Medium Enterprise) | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 0 | 0 |
| | Kiwanda Kikubwa (Large Enterprise) | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | | | **186** | **626** |

| Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanyakazi | Mtaji Uliowekezwa katikaMitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| **MPIMBWE DC** | Kiwanda Kidogo Sana (Micro Enterprise) | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 166 | 191 |
| | Kiwanda Kidogo (Small Enterprise) | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 47 | 276 |
| | Kiwanda cha Kati (Medium Enterprise) | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 11 | 345 |
| | Kiwanda Kikubwa (Large Enterprise) | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 2 | 120 |
| **Jumla** | | | | **226** | **932** |
| **JUMLA KUU (MKOA)** | | | | **1,934** | **6,378** |

***Muhimu:*** *Endapo kigezo cha mtaji kitakuwa kikubwa kuliko idadi ya wafanyakazi, basi kigezo cha mtaji kitatumika kutafsiri aina ya kiwanda.*

## 3.0. SEKTA YA BIASHARA

### 3.1. Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa ikama mahitaji ya watumishi wa sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoa wa Katavi ni 45, watumishi waliopo ni 27, upungufu ni 18 hii ikiwa ni asilimia 60 ya watumishi waliopo. Mchanganuo wa watumishi katika Halmashauri umeoneshwa katika jedwali hapa chini.

| Halmashauri | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Asilimia ya watumishi waliopo |
|---|---|---|---|---|
| Mpanda MC | 9 | 3 | 6 | 33 |
| Nsimbo DC | 9 | 7 | 2 | 78 |
| Mlele DC | 9 | 5 | 4 | 56 |
| Mpimbwe DC | 9 | 6 | 3 | 67 |
| Tanganyika DC | 9 | 6 | 3 | 67 |
| **JUMLA** | **45** | **27** | **18** | **60** |

### 4.**1.1 Idadi ya Wafanyabiashara na Makusanyo ya Mapato mwaka 2021 hadi Februari, 2026**

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Februari, 2026 idadi ya wafanyabiashara walipa kodi imeongezeka toka 5,518 hadi 10,376 mwezi Februari 2026 sawa na ongezeko la asilimia 27.72

Aidha, kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na shughuli za biashara hadi mwezi Februari ni Tshs. 3,145,038,139.45. Jedwali hapa chini limechanganua kwa kila Halmashauri kama ifuatavyo;

| Halmashauri | Idadi ya Wafanyabiashara hadi Juni,2025 | Idadi ya Wafanyabiashara hadi Februari, 2026 | % Ongozeko la wafanyabiashara | Fedha zilizokusanywa hadi June,2025 | Fedha zilizokusanywa hadi Februari 2026 | % Ongozeko la Makusanyo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mpanda MC | 2,290 | 3,398 | 21.8 | 3,896,308,390.11 | 2,139,884,195.45 | (45) |
| Nsimbo DC | 1,563 | 1,930 | 34.5 | 359,265,142.00 | 387,131,962.00 | 7.76 |
| Tanganyika DC | 2,252 | 2,290 | 1.68 | 299,099,127.00 | 324,985,702.00 | 8.65 |
| Mlele DC | 1,096 | 1,170 | 6.75 | 135,334,500 | 158,904,500.00 | 17.42 |
| Mpimbwe DC | 923 | 1,588 | 72.04 | 74,460,350.00 | 134,131,780.00 | 80.14 |
| JUMLA | 8,124 | 10,376 | 78.3 | 4,764,467,509.11 | 3,145,038,139.45 | (33.99) |

**4.1.1 Mchango wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mapato ya Halmashauri.**

Katika mwaka wa fedha wa 2025/2026 kufikia mwezi Februari 2026 sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji kupitia vyanzo mbalimbali imechangia kiasi Tshs. 3,145,038,139.45 katika makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri hii ikiwa ni asilimia 18.19 ya uchangiaji wa sekta katika makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Mchanganuo ni kama jedwali lifuatalo linavyochanganua;

| Jina la Halmashauri | Makusanyo ya H/W kwa mwaka 2025/26 kufikia Februari,2026 | Kiasi kilichokusanywa kutoka vyanzo vya sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji hadi Februari, 2026 | % ya Mapato yaliyokusany wa toka sekta viwanda, biashara na uwekezaji |
|---|---|---|---|
| **Mpanda MC** | 3,531,375,355.69 | 2,139,884,195.45 | 12 |
| **Nsimbo DC** | 1,879,246,769.84 | 387,131,962.00 | 38.6 |
| **Tanganyika DC** | 7,494,683,692.67 | 324,985,702.00 | 1.2 |
| **Mlele DC** | 1,853,367,336.00 | 158,904,500.00 | 3.4 |
| **Mpimbwe DC** | 2,532,958,404.82 | 134,131,780.00 | 10.7 |
| **JUMLA** | 17,291,631,559.02 | 3,145,038,139.45 | 18.19 |

### 4.1.1 Makisio ya Idadi ya Wafanyabiashara na Makusanyo ya Mapato kwa mwaka 2025/26

**K**atika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi mwezi Juni, 2026 makisio ya wafanyabiashara watakao ongezeka ni 1,064 ambayo ni sawa na asilimia 13 ya ongezeko ikilinganishwa na mwaka 2024/25. Aidha, makisio ya makusanyo ya fedha kutokana na ongezeko la wafanyabiashara ni Tshs. 796,376,067.19. Mchanganuo wa makisio haya ni kama unavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

| Halmashauri | Idadi ya Wafanyabiashara hadi Juni 2025 | Makisio ya Wafanyabiashara watakao ongezeka hadi Juni 2026 | % Ongozeko la wafanyabiashara | Makisio ya mapato yatakayokusanywa kutokana na ongezeko la wafanyabiashara hadi Juni, 2026 |
|---|---|---|---|---|
| **Mpanda MC** | 2,290 | 400 | 17 | 100,000,000.00 |
| **Nsimbo DC** | 1,563 | 103 | 8 | 39,733, 542.00 |
| **Tanganyika DC** | 2,252 | 118 | 5 | 121,500,000.00 |
| **Mlele DC** | 1,096 | 106 | 10 | 41,910,000.00 |
| **Mpimbwe DC** | 923 | 337 | 37 | 632,966,067.19 |
| **JUMLA** | 8,124 | 1,064 | 13 | 796,376,067.19 |

### 4.1.1 Orodha ya vyanzo vipya vya mapato vitakavyoanzishwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha 2025/26 wataalam wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji kwa kushirikiana na wataalam wengine wamepanga kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kama ifuatavyo;

| **Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda** | | | |
|---|---|---|---|
| **SN** | Jina la chanzo kipya cha mapato | Jina la Kata chanzo kipya kitapoanzishwa | Jina la Kijiji/Mtaa chanzo kipya kitapoanzishwa |
| **1.** | Ushuru wa maegesho | Kashaulili na Majengo | Kashaulili na Majengo |
| **2.** | Kodi ya Vibanda | Mpanda Hotel | Mpanda Hotel |
| **3.** | Ushuru wa Uchafuzi wa Mazingira | Uwanja wa ndege, Magamba na Misunkumilo | Uwanja wa ndege, Magamba na Misunkumilo |

| Halmashauri ya Wilaya Mlele | | | |
|---|---|---|---|
| **SN** | Jina la chanzo kipya cha mapato | Jina la Kata chanzo kipya kitapoanzishwa | Jina la Kijiji/Mtaa chanzo kipya kitapoanzishwa |
| **1.** | Stendi ya Malori | Inyonga | Inyonga |
| **2.** | Soko la Bidhaa Mchanganyiko | Inyonga | Kalovya |

| Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe | | | |
|---|---|---|---|
| **SN** | Jina la chanzo kipya cha mapato | Jina la Kata chanzo kipya kitapoanzishwa | Jina la Kijiji/Mtaa chanzo kipya kitapoanzishwa |
| **1.** | Uuzaji wa tofali | Usevya - Kiwanda cha matofali | Usevya |
| **2.** | Ushuru wa probox na Mabasi | Usevya-stendi | Usevya |

| Halmashauri ya Tanganyika | | | |
|---|---|---|---|
| **SN** | Jina la chanzo kipya cha mapato | Jina la Kata chanzo kipya kitapoanzishwa | Jina la Kijiji/Mtaa chanzo kipya kitapoanzishwa |
| **1.** | Leseni za wakandarasi wanaojenga barabara | Kata za Kabungu, Kasekese, Karema, Sibwesa na Tongwe | Kabungu, Kasekese, Karema, Sibwesa na Majalila |

| Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo | | | |
|---|---|---|---|
| **SN** | Jina la chanzo kipya cha mapato | Jina la Kata chanzo kipya kitapoanzishwa | Jina la Kijiji/Mtaa chanzo kipya kitapoanzishwa |
| **1.** | Standi ya mabasi NSIMBO | Kapalala | Songambele |
| **2.** | Standi ya mabasi ya Magula na soko jipya la Magula. | Sitalike Mtisi | Sitalike Mtisi |

## 5.0 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

### 5.1. Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mahitaji ya watumishi wa TRA Mkoa wa Katavi ni 87 watumishi waliopo ni 79 upungufu ni 8 hii ni kwa asilimia 9.2 ya watumishi waliopo.

### 5.2 Idadi ya Walipa kodi na Makusanyo

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Februari 2026, idadi ya walipakodi kupitia TRA Mkoa wa Katavi imeongezeka toka 8,125 mwaka 2021 hadi 23,274 kufikia Februari 2026. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 186.45. Makusanyo ya kodi yameongezeka toka shs 7,235,421,323.19 mwaka 2021 hadi shs. 54,853,242,728.22 mwezi Februari 2026 sawa na ongezeko la asilimia 108.09 ikilinganishwa na makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano ya nyuma.

### 5.3 Makusanyo ya mapato kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026.

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Juni, 2026 TRA Mkoa wa Katavi imepangiwa kukusanya kiasi cha shilingi 19,971,679,891.83 ambapo hadi Februari 2026 kiasi kilichokusanywa ni shilingi 15,329,318,752.44 sawa na asilimia 118.01 ya lengo la kukusanya shilingi 12,989,342,348.87 hadi Februari 2026 kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

| MWEZI | Lengo (TZS) | Kiasi kilichokusanywa (TZS) | Kiwango cha utendaji kazi (%) |
|---|---|---|---|
| Julai 2025 | 1,435,374,500.00 | 1,836,906,416.61 | 127.97% |
| Agosti 2025 | 1,367,100,000.00 | 1,559,991,445.55 | 114.11% |
| Septemba 2025 | 1,758,584,500.00 | 2,135,019,706.83 | 121.41% |
| Oktoba 2025 | 1,450,223,088.89 | 1,856,206,559.48 | 127.99% |
| Novemba 2025 | 1,337,780,259.98 | 1,796,378,011.97 | 134.28% |
| Desemba 2025 | 2,423,500,000.00 | 2,581,120,707.24 | 106.50% |
| Januari 2026 | 1,568,950,000.00 | 1,738,251,320.95 | 110.79% |
| Februari 2026 | 1,647,830,000.00 | 1,825,444,583.81 | 110.78% |
| **JUMLA KUU** | 12,989,342,348.87 | 15,329,318,752.44 | 118.01% |

## 6.0 Wakala wa Vipimo (WMA)

### 6.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama ya Wakala wa Vipimo (WMA) mahitaji ya watumishi wa WMA Mkoa wa Katavi ni 6 watumishi waliopo ni 6 na kufanya kuwa na utoshelevu wa watumishi wa taasisi hii.

### 6.1.1 Utekelezaji wa Shughuli

Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi Februari, 2026 Wakala wa Vipimo Mkoa wa Katavi umefanya ukaguzi katika jumla ya vipimo 38,482 kati hivyo vipimo vilivyobainika kuwa na kasoro ni 1,094 kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na faini na tozo mbalimbali toka mwaka 2021 hadi Februari, 2026 ni Tshs. 1,108,177,384.00. Aidha, vipimo vilivyofanyiwa ukaguzi toka Julai 2025 hadi Februari 2026 ni 9,014 kati ya hivyo vipimo vilivyobainika kuwa na kasoro ni 348 kiasi kilichokusanywa kutokana na faini na tozo ni Tshs. 231,773,438.00. Matokeo ya ukaguzi uliofanywa na Wakala wa Vipimo yamefanya wafanyabiashara wamekuwa na mwitikio wa kutumia vipimo sahihi.

### 6.1.2 Shughuli zitakazotekelezwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha wa 2025/26 Wakala wa Vipimo Mkoa wa Katavi unakusudia kufanya ukaguzi katika jumla ya vipimo 6,444 na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wafanyabiashara wapatao 6,310 na kwa wananchi 31,550. Ofisi ya Wakala wa Vipimo Katavi itaendelea kufanya kaguzi mbalimbali na kutoa elimu ya matumizi ya vipimo sahihi kwa wananchi na wafanyabiashara.

# 7.0 SEKTA YA BANDARI

## 7.1 Idadi ya Watumishi

Kwa sasa Bandari ya Karema ina jumla ya watumishi wa umma 7.

### 7.1.1 Utekelezaji wa Shughuli

Bandari ya Karema imeanza kutumika Septemba Mosi, 2022 hadi Februari, 2026, tani zilizopitia Bandari ya Karema ni tani 17,265 za mzigo mchanganyiko, kiasi cha fedha kilichokusanywa ni Tshs. 362,379,698.12. Pia bandari imehudumia jumla ya abiria 10,909 waliotumia bandari kwa kusafiri. Aidha, meli tisa (9) na Boti 659 zimetumia bandari ya Karema.

### 7.1.2 Ujenzi wa Meli nne (4) za mizigo

Mnamo tarehe 12 Desemba 2024, TPA iliingia mkataba na Kampuni ya Kichina ya Gold Voyage Logistics, Kampuni tanzu ya Kampuni kubwa ya Madini duniani ya ZIJIN MINING GROUP yenye Makao Makuu yake huko China. Utekelezaji wa Mkataba huu ni wa miaka miwili (2) ambao utekelezaji wake umeanza rasmi tarehe 1 Aprili 2025. Kwa mujibu wa mkataba Kampuni itajenga jumla ya meli nne (4) za migizo zenye uwezo wa kubeba tani 2,000 kila moja. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ujenzi wa meli mbili (2) umefikia asilimia 100 na meli moja ujenzi umefikia asilimia 95 na meli nyingine ujenzi umefikia asilimia 90.




*Bandari ya Karema*



*Meli ziliundwa katika Bandari ya Karema*

## 8.0 SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

### 8.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama watumishi wanaotakiwa katika uwanja wa ndege wa Mpanda ni 31 watumishi waliopo ni 24 upungufu ni 7 hii ikiwa ni asilimia 77 ya watumishi waliopo.

### 8.1.1 Utekelezaji wa Shughuli

Huduma ya usafiri wa anga Mkoani Katavi ilianza kutolewa tarehe 26 Oktoba 2019, tangu kipindi hicho hadi Februari, 2026 idadi ya wasafiri imeongezeka kutoka 5,721 mwaka 2019 hadi 78,026 Februari, 2026. Idadi ya siku za kusafiri ni mara tatu kwa wiki yaani siku ya Jumanne, Alhamisi na Jumamosi. Kiasi cha fedha kilichokusanywa kimeongezeka toka Tshs.64,274,000.00 mwaka 2019 hadi Tshs. 802,418,616.41 Februari, 2026.




***Ndege -Kampuni ya ATCL ambayo hutoa huduma za Usafari wa Anga***




**Uwanja wa Ndege wa Mpanda**

## 9.0 SEKTA YA MADINI

### 9.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama watumishi wanaotakiwa katika Ofisi ya Afisa Madini Mkazi ni 22 watumishi waliopo ni 22 upungufu ni 0 hii ikiwa ni asilimia 100 ya watumishi waliopo.

#### 9.1.1 Idadi ya Migodi

Mkoa wa Katavi umejaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali kama vile dhahabu, shaba, Galena, Fedha (Silver), Nickel, Mangenese nk. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Februari, 2026 ni kuongezeka kwa idadi ya migodi toka 911 mwaka 2021 hadi 2,038 Februari 2026, kati hiyo migodi mikubwa ni 0, migodi ya kati ni 16 na migodi midogo ni 2,022 Idadi ya Watanzania waliojipatia ajira kutokana na shughuli za madini ni zaidi ya 25,000 wengine wana ajira ya kuduma na wengine wana ajira za mikataba.

#### 9.1.2 Soko la Madini la Mpanda

Soko la madini Mkoa wa Katavi lilianzishwa mwezi Mei, 2019 katika Manispaa ya Mpanda. Jumla ya mauzo ya dhahabu hadi Februari, 2026 ni gramu 1,584,653.17 gramu hizo zina thamani ya Tsh. 201,799,766,012.18. Aidha, mrabaha uliokusanywa ni Tsh. 11,490,158,146.26, ada ya ukaguzi (clearing and inspection fee) kiasi cha Tsh. 1,718,841,565.24 na ushuru wa huduma Tsh. 728,119,885.06 zilipelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ya Nsimbo, Tanganyika na Manispaa ya Mpanda.

### 9.2.1 Biashara ya Makinikia

Tani za makinikia zilizosafirishwa nje ya nchi hadi Februari, 2026 ni tani 34,964.08 zikiwa na thamani ya Tsh. 274,711,352,532.68 ambapo Mrabaha wa Tsh. 16,078,871,266.38 ulikusanywa na ada ya ukaguzi Tsh. 2,224,290,606.19 ilikusanywa.

9.1.2 Makusanyo ya fedha yatokanayo na shughuli za madini
Makusanyo ya fedha yatokanayo na shughuli mbalimbali za madini yameongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonyesha katika kwenye jedwali hapa chini.

| Mwaka | Lengo la Makusanyo (Tsh) | Makusanyo Halisi(TShs.) | Asili mia (%) |
|---|---|---|---|
| 2017/18 | 1,000,000,000 | 1,168,993,197.78 | 117 |
| 2018/19 | 1,000,000,000 | 629,052,950.41 | 63 |
| 2019/20 | 1,000,000,000 | 2,273,544,321.53 | 227.4 |
| 2020/21 | 1,250,000,000 | 6,294,174,783.03 | 504 |
| 2022/23 | 7,488,000,000 | 4,389,810,305.85 | 59 |
| 2023/24 | 6,850,000,000 | 6,180,025,156.38 | 90.2 |
| 2024/25 | 7,000,000,000 | 9,261,668,258.27 | 132.2 |
| 2025/26 (Febr.) | 10,000,000,000 | 7,658,664,906.62 | 76.59 |
| JUMLA | 35,588,000,000 | 37,855,933,879.71 | |

***Jedwali : Takwimu za Makusanyo ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 hadi Februari 2025/26***

Kutokana na takwimu tajwa hapo juu makusanyo yote ya fedha yaliyopatika kupitia sekta ya madini Mkoa wa Katavi toka mwaka 2021 hadi Februari, 2026 ni Tshs 37,855,933,879.71.

### 9.1.2 Fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini.

Ili kuvutia wawekezaji wakubwa na wa kati Mkoa umejipanga kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya madini. Maeneo muhimu ambayo wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza yamechanganuliwa katika jedwali lifuatalo;

| SN | Aina ya Uwekezaji | Jina la Kijiji | Taratibu za kufuata ili kuanza uwekezaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Mitambo ya uyeyushaji wa madini (Smelters) | Eneo lolote ndani ya Mkoa Mwekezaji atakalopenda | Mwekezaji afike Ofisi ya Afisa Madini Mkaazi (RMO) –Katavi. |
| 2. | Maghala ya kuuzia baruti (Explosive Mgazine). | Eneo lolote ndani ya Mkoa Mwekezaji atakalopenda | Mwekezaji afike Ofisi ya Afisa Madini Mkaazi (RMO) –Katavi. |

## 10. SHIRIKA LA VIWANGO (TBS)

10.1. Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama watumishi wanaotakiwa katika Ofisi ya Kanda ya Shirika la Viwango (TBS) ni 18 watumishi waliopo ni 13 upungufu ni 5 hii ikiwa ni asilimia 72 ya watumishi waliopo.

### 10.1.2 Utekelezaji wa Shughuli

Kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi mwezi Februari, 2026 idadi ya viwanda vilivyokidhi vigezo na kupata vyeti vya ubora wa bidhaa Mkoa wa Katavi imeongezeka toka 18 mwaka 2021 hadi 48 Februari, 2026. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2025/26 Shirika la Viwango limepanga kutoa vyeti vya ubora wa bidhaa kwa viwanda 10 vitakavyokidhi vigezo vya ubora Mkoani Katavi.

Pia katika kipindi cha mwaka 2022 hadi Februari, 2026 Shirika la Viwango kupitia ofisi ya Kanda ya Magharibi limetoa elimu kwa wadau 242 wa biashara mbalimbali za uchakataji, uzalishaji na ufungashaji wa bidhaa. Mchanganuo wa idadi ya wadau waliopewa mafunzo, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ni wadau 109, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ni wadau 49, Tanganyika wadau 43, Nsimbo wadau 41.

## 11.1 HITIMISHO

Mkoa wa Katavi umejipanga kikamilifu kuvutia wawekezaji na kukuza biashara kwa kuandaa Mazingira rafiki kwa wawekezaji na Wafanyabiashara ili kuinua Uchumi na Ustawi wa maendeleo ya Mkoa na Tanzania kwa Ujumla.